



***Mkuu wa Mkoa Singida Dkt. Binilith  
Mahenge (katikati) akikata utepe  
kuashiria ufunguzi wa Zahanati ya Kijiji  
cha Maweni wilayani Manyoni***

*Imewekwa mtandaoni .sept 22/2021*

Mkuu wa Mkoa wa Singida Dkt Benilithi Mahenge amewapongeza wananchi wa Kijiji cha maweni kwa kujitoa kujenga zahanati ya Kijiji.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa zahanati hiyo terehe 21/2/2021 Mkuu wa Mkoa wa Singida Dkt Benilithi Mahenge amesema kuwa ni hatua kubwa sana

Mahenge amesema kuwa ni vigumu sana kwa Wananchi waliowengi kujitoa kama ambavyo wamefanya wananchi wa Kijiji cha Maweni.

“Nataka niwapongeze sana wananchi wa Maweni kwa juhudini mlizozionesha kitendo cha kuanza kujenga jengo hili na Serikali ikaona maana bila wao kuanza hata Serikali isingejua kama kuna kazi inafanyika hapa juhudini walizozionesha ni kubwa sana hizo fedha mlizotoa, million, 9 ni nyingi sana kwa hali walizonazo wananchi hawa” alisema Dkt Mahenge.

Aidha niwapongeze sana uongozi wa Wilaya ya Manyoni ,Halmashauri pamoja na Chama cha Mapinduzi kwa jinsi amabavyo wanashirikiana na Serikali kwa kuendelea kuleta maendeleo pamoja na kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi

Dkt Mahenge aliongeza pongezi kwa Chama cha Mapinduzi chini ya Mwenyekiti wa CCM Wilaya pamoja na Mh Mbunge kwa jinsi ambavyo wanajitoa katika ufuatliaji wa kusimamia maendeleo ya Jimbo la Manyoni pamoja na maendeleo ya miradi yote.

Hata hivyo amewataka wananchi kumpongeza sana Mh Raisi Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo ameendele kuendleeza miradi mablimbali ikiwemo miradi ya ujenzi wa zahanati na vituo vya afya pamoja na miradi mingine ya maji .

“Ombi langu kwenu wananchi na hasa kina mama mnakumbuka katika kampeni za kuzitafuta kura Mh Rais Samia Suluhu hasan alisimama kidete kuwatetea wakina mama katika suala zima la maji na afya akasema tumtue mama ndoo lakini tuhakikishe akina mama hawapati taabu katika suala la afya naomba tumpigie sana mama makofi” alisema Dkt Mahenge

Naye Mkurugenzi wa Halmshauri ya Wilaya ya Manyoni Melkzedeki Humbe amesema kuwa tayari wamepatikana wahudumu wa afya katika zahanati hiyo na kwamba mmoja wapo anatarajia kuwasili pia hivi karibuni mara tu atakapohitimu masomo yake ili kuweza kuongeza nguvu kazi katika kutoa huduma katika zahanati hiyo.

“Niseme tu katika bajeti ijayo tutatenga fedha kwa ajili ujenzi wa majengo yaliyosalia ya watumishi ambao watapaswa kuishi hapa” alisema Humbe.

Kuhusu suala la maji katika zahanati hiyo Mwenyekiti wa Halmshauri ya Wilaya ya Manyoni Jumanne Mlagaza alisema kuwa zahanati hiyo itakuwa ikitumia maji kutoka mradi wa maji wa kintinku lusilie ambapo awamu ya kwanza tayari imeteklezeka na mpaka kufikia sasa zoezi la ni ulazaji wa mabomba unaendelea ili kuweza kusaidia maji kufika katika vijiji hivyo kikiwepo Kijiji cha maweni

“Nimpongeze Mkoo wa Mkoa na Mh Mbunge kwa juhudini walizonesha katika kufuatlia mpaka sasa mradi unatarajia kupoea Tsh bilioni mbili ili kuweza kukamilisha awamu ya pili ambapo itasaidia vijiji vyote ikiwemo maweni kupata maji niwapongeze sana” alisema Mlagaza

Kuhusu suala la Ichf iliyoboreshwa Mahenge aliwataka wananchi kuiga mfano wa mzee aliyekata bima ya afya ili waweze kutibiwa kwa haki na usawa na kupata huduma bora.

“Ukitaka kufaidi mab ilion ya fedha ambayo ametoa Mh Rais Samih Suluhu Hassani katika kuboresha sekta ya afya ni wewe kukata bima ya afya utatibiwa bure madawa utapa ta bure hiyo ndiyo nia ya kufaidi haya mabilion aliyatoa Mh Raisi”alisema Dkt Mahenge.

Kuhusu suala la chanjo Dkt Mahenge amewahimiza wananchi kuendelea kujitokeza kumuunga mama mkono katika suala I chanjo ili kuendelea kujilinda na maambukizi ya uviko 19.

“katika vitu ambavyo mama Samia ameuonyesha upendo wake kwa wananchi kuruhusu chanjo Na amewataka wananchi kutambua kuwa sehemu zote zinazotoa huduma za afya na hapa maweni ipo nawaombeni wananchi wangu tuende tukachanje tumuunge Mh Rais kutengeneza nguvu kazi ya kila mchapakazi ni kwena kuvchnja nendeni mkachanje”alisema Dkt mahenge.

Katika hatua nyingine Dkt Mahenge amewataka vijana kutumia technlogia ya mitandao ya simu kutafuta masoko ya bidhaa zao badala ya kutegemea Serikali kufanya kila kitu

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa mradi wa wafuganyuki wa kisasa wa kjiji cha muhalala Dkt Mahenge amewataka vijana

kuhakikisha kwamba amewataka vijana kuhakikisha kwamba wanatumia uwepo wa simu na mitandao ya kijamii kwa lengo la kuuza na kununua bidhaa mbalimbali.

Alisema Serikali imetumia fedha nyingi kuwekeza miundombinu mbalimbali ikiwemo mkongo wa Taifa ili kulinda kundi la vijana lipate maarifa mapya ya kibashara .

“Hivyo kwa kuliona hili niwaombe vijana kulinda miundombinu pamoja na miradi wanayotafutiwa na mashirika mbalimbali pamoja na Serikali ili kufikia lengo la kuwakomboa vijana wengi waliyo[po katika makundi ya wanawake na wanaume.alisema Dkt Mahenge.

Aidha Dkt Mahenge amebainisha kwamba Serikali inatekeleza sheria inayozitaka Halmashauri kutenga asilimia kumi 10% kwa ajili ya vijana na asilimia 40% kwa ajili ya wanawake na walemavu .na kwa kupita hilo amemwagiza mkurugenzi wa halamashauri melkzedek humbe kuhakikisha kwamba asilimi hiyo inatumika kuwaendeleza vijana wa manyoni.

Na katika ziara yake Dkt Mahenge ametembelea na kukagua miradi ya EP4R ambayo ni madarasa ya ,shule ya sekodari na madrasa katika shule ya msingi sayuni.



**vifaa vijana Wajasriamali walivyowezeshwa Mkuu wa wilaya ya Manyoni Rahabu Mwagisa  
akizungumza wakati wa hafla ya kuwakabidhi na Shirika la Compassion International  
Tanzania (CIT)**



**Askofu Elisante Mwenegoha wa Kanisa la Tanzania Assemblies of God (TAG) akizungumza  
wakati wa hafla ya kukabidhi vifaa hivyo.**



**Mkuu wa Mkoa Singida Dkt. Binilith Mahenge akiangalia baadhi ya vifaa waliokabidhiwa vijana hao na Shirika la Compassion International Tanzania (CIT)**



**. Mkurugenzi mtendaji wa Halmshauri ya Wilaya ya Manyoni Melkzedek Humbe akizungumza wakati wa uzinduzi wa zahanati ya kijiji cha Maweni**



**Mbunge wa jimbo la manyoni mashariki Dkt Pius Chaya akizungumza kwenye hafla hiyo**



**Dkt Mahenge akimkabidhi kadi ya bima ya afya iCHF iliyoboreshwa mzee Godwin Nguruga**



S

**Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni Jumanne Mlagaza  
akifafanua juu ya maji yatakavofika katika Kijiji hicho na hadi kwenye zahanati  
hiyo**



**Wananchi waliojitekeza kushuhudia uzinduzi wa zahanati ya Kijiji cha  
Maweni wakisikiliza taarifa ya ukamilishwaji wa zahanati hiyo  
iliyokuwa ikisomwa na Mganga Mkuu wa Wilaya ya Manyoni Dkt  
Furaha Mwakafwila mbele ya Mkuu wa Mkoa**